JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu Na: +255 (026) 2963309/13/14
Nukushi: +255 (026) 2963316
Barua Pepe: ps@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
2 Mtaa wa Ardhi,
S.L.P. 2908,
**40477 DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

## UFAFANUZI WA NOTISI ZILIZOTOLEWA KWA VIJIJI VYA OLOLOSOKWAN, SOITSAMBU, ENGUSEROSAMBU, ARASH NA LOSOITO

**13 Julai, 2026, Dodoma**

Wizara inapenda kutoa ufafanuzi kutokana na taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu notisi zilizotolewa tarehe 4 Juni,2026 na Ofisi ya Msajili wa Hati Mkoa wa Arusha kwa Vijiji vya **Ololosokwan, Soitsambu, Enguserosambu, Arash na Losoito** vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro Mkoani Arusha.

Notisi zilizotolewa zililenga kurekebisha Daftari la Msajili ili kuondoa kumbukumbu za usajili wa Hatimiliki zilizotolewa kwa Vijiji hivyo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114.

Utaratibu wa kurekebisha Daftari la Kumbukumbu za Usajili ulilenga kuondoa Hatimiliki na kubakisha Cheti cha Ardhi ya Kijiji kinachotoa mamlaka kwa Halmashauri za Vijiji hivyo kusimamia ardhi kwa ajili ya wanakijiji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114.

Utaratibu huu umekuwa ukitumika katika vijiji vingine nchini vilivyokuwa na Hatimiliki kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura ya 114. Utaratibu wa kurekebisha daftari la usajili utakapokamilika, Vijiji vya **Ololosokwan, Soitsambu, Enguserosambu, Arash na Losoito** vitabaki na vyeti vya ardhi ya Kijiji ambavyo ndio nyaraka rasmi inayoipa halmashauri ya vijiji vyao mamlaka ya kusimamia ardhi kwa manufaa ya wanakijiji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114**.**

Wizara inawataka wananchi kupuuza upotoshaji wowote unaotolewa kuhusiana na mchakato huo kwamba unania ya kuchukua ardhi za Vijiji tajwa na kuipeleka kwenye Mamlaka nyingine ya usimamizi, Mwekezaji au mwananchi yeyote.

Imetolewa na

Eleuteri Mangi

**MKURUGENZI WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**